



## Tulikatazwa kusindikiza jeneza, na hatukusisitiziwa katazo hilo

Kutoka kwa Ummu Atwiya radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake amesema:  
Tulikatazwa kusindikiza jeneza, na hatukusisitiziwa katazo hilo.

[Sahihi] [Wamekubaliana Bukhari na Muslim juu ya usahihi wake]

Anaeleza Ummu Atwiya Muanswari (mzaliwa wa Madina) radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, ya kwamba Mtume rehema na amani ziwe juu yake aliwakataza wanawake kusindikiza jeneza; na hii ni kwa sababu ya mitihani inayohofiwa juu yao, na uchache wa subira yao, kisha akaeleza radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake kuwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake hakutilia mkazo katika katazo hili kama anavyofanya katika matakazo mengine.

<https://www.sunnah.global/hadeeth/sw/show/3228>

النجاة الخيرية  
ALNAJAT CHARITY

